**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**
**Mkuu wa Shule: 0756510222/0656384329**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0626660573/0765890282**
**Mhasibu wa Shule: 0757142467/0621006663**
**Matron/Patron: 0752402811**

**Shule ya Sekondari Matai,**

**S.L.P. 75,**

**Matai – Kalambo.**

**Julai, 2024.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**..................................................**
**S.L.P ..........................................**
**..................................................**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATAI HALMASHAURI YA KALAMBO MKOA RUKWA MWAKA 2024/2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya ............

Shule ya Sekondari Matai ipo umbali wa Kilometa 2 Kusini/Mashariki mwa Mji wa MATAI, Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi Sokomatola (STANDI YA ZAMANI SUMBAWANGA MJINI) Nauli ni Shilingi 3000 .NA kwa pikipiki ni shiligi 2000 kutoka matai mjini mpaka shuleni na Shilingi .2000 kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe Julai, 2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suruali ya lightblue

na kaki

**Maelezo ya mshono suruali**

ii. iwe pana chini na iwe na sellebration.

iii. Mashati …2 meupe mikono mirefu.

iv. Sare ya Michezo ni trucksuti nyeusi

jozi moja na raba za michezo jozi moja rangi yoyote.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

viii. Sweta …mbili za blue

ix. Nguo za kushindia trucksuti moja ya light blue.

x. Tai mbili ya lightblue na kaki zinazoendana na rangi za suruali.

xi. Tisheti (T-shirt) mbili zenye rangi ya damu ya mzee

zenye kola.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari TISA COUNTER BOOK QR 3.

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe la nchi mbili na nusu.
vi. Mashuka ya rangi ya lightblue Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.
vii. Nguo za ndani za kutosha.
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

**ANGALIZO**: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

## 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** MICHANGO HII IWEKWE KWENYE **AKAUNTI NAMBA 62101100048 JINA MATAI SECONDARY SCHOOL SELF-RELIANCE.**

# 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)**.

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**Karibu sana katika shule hii**

..........................

**PIUS I. KWIMBA**

**Mkuu wa Shule.**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ........................

The Headmaster
Matal Sec. School
P.O. Box 75, Kalambo

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0756510222/ 0656384329**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0626660573/ 0765890282**
- **Mhasibu wa Shule: 0757142467/ 0621006663**
- **Mwandamizi Taalum: 0768060257/ 0769296469**
- **Mwandamizi Malezi: 0765093709**

MATAI SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 75,
KALAMBO - RUKWA.

DATE:.............................................
MEDICAL OFFICER:
.....................................................
.....................................................
.....................................................

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine the above named as to His/ Her fitness as indicated below. Arrange for necessary treatment so that the certificate may be signed and brought to school by the student.

This certificate must be signed by a qualified medical officer of recognized Hospital
......................................................................................................

## MEDICAL CERTIFICATE.

I have examined the above named student with regard to:-

Skin:.............................................Abdomen ...............................
Eyes: ...........................................Urine: .....................................
Teeth: ......................................... Hemoglobin: ............................
Spleen: ........................................ Chest: ....................................

Any Disabilities:..........................................................................

I consider that:-
He is in good health free from infections, and fit to come to school

He is fit come to school after having:.........................................................
Treatment for: ..................................................................................

Name & Signature ......................................................Date.....................

MEDICAL OFFICER

The Headmaster
Matai Sec. School
P.O. Box 75, Kalambo

## SHULE YA SEKONDARI MATAI – KALAMBO

## FOMU YA KUANDIKISHA HABARI ZA MZAZI.

Jina Kamili: ............................................................................

Tarehe ya Kuzaliwa: .......................................................

Mahali pa kazi: ..............................................................

Dini: ................................................................................

Uraia: ..............................................................................

Wilaya ya Nyumbani: .....................................................

Simu ya Baba: ..................................................................

Simu ya Mama: .................................................................

Simu ya Mtendaji wa Mtaa Au Kijiji: ..................................

Maelezo mafupi kuhusu Afya ya Mwanafunzi: ......................

..........................................................................................

..........................................................................................

Nathibitisha kuwa Taarifa nilizotoa Hapo Juu Ni Kamili Na Kweli.

The Headmaster
Matal Sec. School
P.O. Box 75, Kalambo